30440564

# PROSPECT EXAMS SERIES
## DARASA LA NANE
## KISWAHILI: LUGHA

30442564

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI**

1.Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu kina maswali 50.

2.Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu.

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzoni mwa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C. D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi.Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

Katika kijitabu cha maswali:

**20.** Kanusha.

Kujali kwangu kumenisaidia

A. Kutojali kwangu kutomenisaidia
B. Kutojali kwangu kujanisaidia
C. Kutojali kwangu hakujanisaidia
D. Kujali kwangu kutomenisaidia

Jibu sahihi ni C

**Katika karatasi ya majibu:**

1. [A] [B] [C] [D] 10. [A] [B] [C] [D] 20. [A] [B] [C] [D] 30. [A] [B] [C] [D] 40. [A] [B] [C] [D]

katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 20, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Prospect Publishers
@prospectpulishers14@gmail.com

© *Published and printed by Prospect Educational Publishers*

**Geuza Ukurasa**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Sitausahau mwaka wa elfu mbili na kumi. Mashindano ya Kombe la Dunia ___1___ Ijumaa mwezi Aprili. Mchezo huu wa ___2___ ndio mchezo ___3___ kote duniani ___4___ unapendwa na watu wa umri, jinsia, dini, maeneo na ___5___ mbalimbali. Mashabiki walingoja kinyang'anyiro chenyewe kwa ___6___ kubwa. Ala zote za muziki ___7___ ___8___ ziliwekwa tayari kwa ajili ya kushangilia ushindi.

1. A. ilianza B. yalianza C. zilianza D. lilianza
2. A. kadanda B. kibemasa C. kubumbu D. kandada
3. A. maarufu B. bora C. bingwa D. pekee
4. A. . B. : C. , D. ;
5. A. mambo B. taifa C. matabaka D. tendo
6. A. shauku B. haramu C. shaka D. kasi
7. A. mathalani B. mithili C. minghairi D. sembuse
8. A. manati, ngoma, kinubi
   B. kimangare, singe, mkwiro
   C. tari, kayamba, tiara
   D. vuvuzela, panda, vigoma

Rafiki ___9___ Abdallah alianza kumfunza ___10___ ya kuendesha baiskeli wakati wa likizo. ___11___ moja baada ya kupata kishuka, Abdallah na rafiki yake wa ___12___ walienda kwenye mlima kuendesha baiskeli yao. Dande alijitapa na kusema, "Nimekuwa bingwa wa baiskeli ngoja uone!" Licha ya rafiki yake kumwonya ___13___ kuendesha baiskeli kwenye mteremko, ___14___ . Alizungusha pedali haraka. Baiskeli ilipoanza kuteremka kwa kasi, aliachilia usukani na kunyanyua mikono juu. Mungu wangu! Alianguka ___15___ mchangani akapoteza fahamu.

9. A. wake B. yake C. naye D. zake
10. A. vile B. mambo C. jia D. jinsi
11. A. Asubuhi B. Adhuhuri C. Alasiri D. Macheo
12. A. kufa kupona B. bure bilashi C. raha mustarehe D. kula kubakishiana
13. A. dhidi ya B. badala ya C. kabla ya D. licha ya
14. A. alikata shauri B. alijitia purukushani C. alirusha roho D. alipanda ngazi
15. A. tifu B. pu C. tapwi D. parr

***Kuanzia nambari 16 hadi 30, jibu kila swali kulingana na maagizo.***

16. Neno "madhumuni" lina silabi ngapi
A. 5 B. 4 C. 7 D. 6

17. Chagua wingi wa sentensi ifuatayo:- Uta na upote wa msasi uliundwa na seremala hodari.
A. Nyuta na pote za wasasi ziliundwa na maseremala hodari.
B. Mauta na maupote ya wasasi yaliundwa na maseremala hodari.
C. Nyuta na pote za masasi ziliundwa na seremala hodari.
D. Uta na upote za wasasi ziliundwa na seremala hodari.

18. Chagua sentensi iliyo sahihi kisarufi.
A. Vitu zingine hazifai kusemwa hadharani.
B. Gari zingine huwa za kifahari.
C. Changu akikaangwa huwa mtamu sana.
D. Samaki zote zilizovuliwa ziliuzwa.

19. Chagua orodha yenye vielezi pekee.
A. Vibaya, aghalabu, chini ya, kefule
B. Jembamba, refu, sita, la kwanza
C. Vibaya, alasiri, kando, njiani
D. Wala, lau, ijapokuwa, licha ya

20. Sentensi "Asingalimwoza binti yake asingalishtakiwa" ina maana kuwa;
A. Alimwoza binti yake kwa kushtakiwa.
B. Hakumwoza binti yake wala kushtakiwa.
C. Hakumwoza binti yake licha ya kushtakiwa.
D. Alishtakiwa kwa kumwoza binti yake.

21. Chagua sentensi ambayo imetumia kinaya.
A. Mateo amekuwa bingwa; alikuwa nambari tatu kuanzia mwisho.
B. Maji ya bahari yalimzungumzia yakamkanya asiogelee.
C. Kwao ni paradiso; wanaishi raha mustarehe.
D. Shehena hiyo ya mizigo ilikuwa nzito kama nanga.

22. Chagua usemi halisi wa sentensi ifuatayo: Tabibu alimwambia mgonjwa kuwa angekuwa akimeza dawa kila siku.
A. Tabibu alimwambia mgonjwa ,"Utakuwa ukimeza dawa kila siku."
B. "Ungekuwa ukimeza dawa kila siku," Tabibu akamwambia mgonjwa.
C. Tabibu akamwambia mgonjwa, "Umekuwa ukimeza dawa kila siku."
D. "Utakuwa ukimeza dawa kila siku, Tabibu alimwambia mgonjwa."

23. $\frac{6}{9}$ kwa maneno ni;
A. Sudusi tisa B. Tusui sita
C. Tusui tisa D. Sudusi sita

24. Chagua sentensi yenye maelezo sahihi.
A. Kufuja ni kutumia mali vibaya ilhali kuvuja ni kupita kwa kitu kiowevu kupitia kijishimo.
B. Doa ni harusi ilhali ndoa ni alama ya kasoro juu ya kitu.
C. Kukonga ni kukusanya vitu au watu mahali pamoja ilhali koga ni sehemu ya nyuma ya kichwa.
D. Sabuni ni madini yanayotumiwa kusafishia nguo ilhali zabuni ni uuzaji wa bidhaa rejareja.

25. Chagua sentensi iliyotumia kiunganishi sahihi.
A. Ilhali alikuwa mgonjwa, alishiriki katika mashindano na akashinda.
B. Lau usingekuja kunieleza, habari hii nisingeijua.
C. Viola alinunua gari bighairi simu?
D. Timu hiyo ni bingwa ikiwa haina mashabiki wengi.

26. Mke na dada wa mume huitana;
A. mitara B. mwanyumba
C. wifi D. wakoi

27. Onyesha sentensi iliyo na dhana ya masharti.
A. Ufisadi ungekomeshwa tungefurahi.
B. Ajira za watoto ni kitendo kibovu.
C. Nendeni mlete vitabu vyenu.
D. Wageni walikuwa wakila nilipofika.

28. Chagua jibu lenye maneno yasiyoambatanishwa ipasavyo.
A. Ndizi - mkungu B. Damu - tone
C. Nywele - shungi D. Barua - msoa

29. Chagua ukanusho mwafaka wa; Mkeka ambao ulitoboka umeshonwa tena.
A. Mkeka ambao haukutoboka haukushonwa tena.
B. Mkeka ambao haukutoboka umeshonwa tena.
C. Mkeka ambao ulitoboka haujashonwa tena.
D. Mkeka ambao haujatoboka haujashonwa tena.

30. Ni methali ipi inayoonyesha kuwa mtu anayechaguachagua sana huenda akaishia kupata kitu kile kibaya?
A. Mtegemea cha nduguye hufa maskini
B. Mtego wa panya huingia waliomo na wasiokuwamo.
C. Mtegemea nundu haachi kunona.
D. Mteua mno huangukia mbovu

***Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali nambari 31 - 40.***

Kwa sasa kuna mifumo miwili ya elimu nchini. Kuna mfumo mpya wa Umilisi na ule wa zamani. Mfumo wa zamani umekuwa wa nane - nne-nne; miaka minane katika shule ya msingi, minne ya sekondari na minne ya taasisi au chuo kikuu. Katika viwango vyote, mitihani ni muhimu sana. Hata hivyo, katika siku za hivi karibuni, mjadala mkali umetokea kuhusu ikiwa mitihani inastahili kuondolewa ama inafaa kubaki.

Awali ya yote ifahamike kuwa mitihani huwa ni kigezo cha kutathmini au kupimia. Mitihani huwawezesha walimu kujua iwapo wanafunzi walielewa vizuri somo au hawakuelewa. Watahiniwa wakifanya mitihani ya kitaifa, serikali huyatumia matokeo ya mitihani hiyo kuamua ni kina nani watakaojiunga na shule zipi.

Lau kusingekuwa na mitihani walimu kwa wanafunzi wasingejitahidi. Mitihani huwafanya wanafunzi na hata walimu kufanya bidii. Hofu ya kufeli mitihani huwafanya wanafunzi kujizatiti, kuwajibika na kusoma kwa mapana na marefu. Katika kusoma na kudurusu huku, maarifa huwaingia akilini na maarifa hayo yatawafaa katika siku za usoni.

Mbali na hayo, mitihani huwawezesha wanafunzi kuvitambua vipawa vyao tangu wakiwa wadogo. Mwanafunzi hujua talanta zake na kuamua kazi ambayo ataisomea na kuifanya atakapokua na kuwa mkubwa. Mathalani, mwanafunzi anayefaulu katika masomo ya Sayansi na Hisabati anaweza akawa daktari, muuguzi, mhandisi au afisa wa kilimo. Bingwa wa uandishi wa insha naye huwa tayari amelitia guu katika bahari ya uandishi, ama wa vitabu, magazeti, majarida au uanahabari.

Ifahamike kuwa mtahiniwa afanyapo mtihani kwa njia moja au nyingine huwa akiwasiliana. Huwa anajaribu kadri ya uwezo wake kunadi maarifa aliyo nayo. Katika siku za usoni, atajua jinsi ya kuyajibu maswali kwa busara, labda katika mahojiano ya kutafuta kazi. Isitoshe, atajua kushawishi watu kama wateja au wampigie kura. Kwa kujua kuandika barua ataweza kuandika barua na kuomba nafasi za kazi au kueleza hisia na mitazamo yao.

Hata hivyo chambilecho wanalugha, hakuna masika yasiyokuwa na mbu. Licha ya manufaa anuwai, mitihani inazo changamoto zake. Kutokana na ushindani mkali, baadhi ya watu huamua kutumia njia za mikato kuipasi mitihani hii. Visa vya wizi wa mitihani vimeongezeka si katika shule za msingi, si sekondari na hata vyuoni. Hata hivi karibuni tumesikia magavana na maseneta waliotumia vyeti visivyo halal!

Kando na hayo, wale ambao kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wao hufeli mitihani, hutaabika maishani. Jamii huwahukumu watu hao. Wengine hupagazwa majina kama 'zuzu', mbumbumbu, fala, jura, gulagula, kisu butu na mengineyo. Watu hao hudunishwa na kujidunisha hadi wanakosa kujithamini. Ipo dhana potovu kuwa kufeli mtihani ni kufeli maisha.

Walimu kwa wanafunzi huwa na shinikizo la kupasi, liwe liwalo. Msukumo huu huwa na athari hasi. Katika baadhi ya skuli, wanafunzi hufungiwa madarasani tangu saa kumi na moja alfajiri hadi saa nne za usiku. Wanafunzi wamenyimwa nafasi ya kucheza au hata kutangamana na wenzao. Kazi hii ya kusoma, kusoma na kusoma inawazuia watoto kukua kikamilifu kimwili, kiakili, kiimani, kimaadili na kijamii.

Pamoja na wengine kuhitimu na matokeo ya kumezewa mate, wahitimu wengi huwa hawajaiva bado! Waajiri wengi wamekuwa wakilalamika kuwa wanapokea wahitimu ambao hawajahitimu hasa. Hili linasababishwa na utamiaji wa njia za mikato za kusoma, mradi wapite mitihani. Wengi huwa wamekaririshwa masomo kikasuku, hawayaelewi hata chembe. Imekuwa elimu tegemezi wala si elimu tekelezi.

Kumbuka, elimu maisha si vitabu. Ni ukweli usiopingika kuwa licha ya changamoto zake, mitihani inao mchango mkubwa sana katika kufaulisha masomo. Hata hivyo, sharti ipigwe msasa na itumike kitaalamu.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza si sahihi kusema kuwa;
A. mfumo wa zamani wa elimu nchini una jumla ya miaka kumi na sita.
B. mitihani huwa ina umuhimu mkubwa katika kufanikisha elimu ya viwango vyote.
C. kuna tofauti ya maoni; wapo wanaothamini mitihani na wengine hawaoni umuhimu wake.
D. mjadala mkali umetokea katika siku za hivi karibuni wa kuiondoa mitihani kabisa.

**32.** Aya ya pili inadhihirisha wazi kuwa mitihani;
A. huwazuia baadhi ya watu kujiunga na taasisi za juu za elimu.
B. ndiyo hutumiwa katika kuwatenganisha wanafunzi wa viwango mbalimbali
C. hutumiwa kwa njia mbaya inayobagua baadhi ya wanafunzi.
D. huwafanya wanafunzi kuelewa waliyofundishwa na walimu

**33.** Kulingana na aya ya tatu;
A. mitihani huwa na mchango mkubwa sana katika kuchochea wadau wote wa elimu kufanya bidii.
B. mitihani isingekuwapo kuna uwezekano mkubwa kuwa walimu wasingefunza hata kidogo.
C. mitihani huwafanya wanafunzi wengi kuhofia na mwishowe wanafeli mitihani.
D. katika kusoma na kudurusu maarifa huwaingia wanafunzi yanayofaa katika mitihani pekee.

**34.** Mitihani;
A. inapokuwa migumu ndipo watu husoma kwa bidii zaidi.
B. inawawezesha walimu kutathmini kiwango cha uelewa wa wanafunzi wao.
C. huwapa nafasi watoto kutambua vipawa vyao wanapokuwa watu wazima.
D. huamua ni tasnia ipi watakayoisomea wanafunzi mnamo siku za usoni.

**35.** Chagua jibu sahihi kulingana na kifungu;
A. Mwanafunzi aliye na ubingwa wa somo la Hesabu na Sayansi anaweza kuwa daktari, mhandisi au afisa wa kilimo pekee.
B. Matokeo ya mtihani humsaidia mwanafunzi kufanya uamuzi wa busara kuhusu taaluma inayomfaa.
C. Waandishi wote wa vitabu, magazeti na majarida huanza kazi hizo tangu wakiwa wanafunzi.
D. Lengo la kipekee la serikali ni kutumia mitihani katika kuamua ni mwanafunzi yupi atakayejiunga na shule ipi.

**36.** Ni methali gani kati ya hizi iliyo na maana sawa na 'hakuna masika yasiyokuwa na mbu' namna ilivyotumiwa kwenye kifungu?
A. Baniani mbaya kiatu chake dawa
B. Siri ya mtungi aijuaye kata
C. Hakuna marefu yasiyokuwa na mwisho
D. Hakuna bamvua lisilo usubi

**37.** Chagua maana ya '**kunadi**' kwa mujibu wa kifungu.
A. Kujumlisha B. Kueleza
C. Kutangaza D. Kuelekeza

**38.** Kwa mujibu wa aya ya saba:
A. mitihani inaweza kufanya baadhi ya watu kutojithamini na kujidhalilisha.
B. mitihani huonyesha wale waliofeli katika maisha kwa kufeli kwenye mitihani.
C. wanaofeli mitihani kwa sababu walizojiletea wao wanyewe hupata taabu katika maisha.
D. majina ya kudunisha wanayopagazwa waliofeli mitihani huwa si sababu ya kuwadhalilisha.

**39.** Kauli, '**huwa hawajaiva bado**' ina maana gani namna ilivyotumiwa katika kifungu?
A. Huwa wamezitumia njia za mikato kupasi kwenye mitihani.
B. Huwafanya waajiri kulalamika sana kulingana na jinsi walivyo.
C. Huwa hawajapata mafunzo barabara kama inavyohitajika kazini.
D. Huwa wamekariri masomo kikasuku na kuwa wanaojitegemea.

**40.** Msimamo wa mwandishi ni kuwa;
A. Licha ya matatizo yake mitihani ina manufaa mengi.
B. Ingawa mitihani ni muhimu changamoto zake ni nyingi kupindukia.
C. Mitihani haina nafasi yoyote katika elimu ya kimamboleo.
D. Mitihani haifai kuwa kiwango cha kutathmini wanafunzi.

**Geuza ukurasa**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41- 50.***

Yamkini nilimfahamu vyema Lorenzo mwaka wa elfu mbili na moja. Awali, nilikuwa nikimwona akiingia tu na kutoka nyumbani mwetu pasipo kuwa na mwao kama nilikuwa na uhusiano wa kinasaba naye. Jinsi tulivyokuwa na mwingiliano mkubwa na binamu, ilikuwa si rahisi kutofautisha nani ndugu wa tumbo moja na yupi wa mjomba, hale na kina shangazi.

Alasiri moja tulifika nyumbani kutoka shuleni. Tulikuwa tukiwahi nyumbani kabla ya watoto wengine wote, sio eti tulikuwa watiifu au tulipenda nyumbani, la hasha! Kutokana na uhaba wa vyakula, kwetu lugha ilikuwa hali ya, akutanguliaye chanoni hukuzidi tonge; chelewa chelewa, ungepata kiporo kimekwanguriwa kikaisha. Kama desturi, tulifululiza mwendo moja kwa moja hadi jikoni. Hata hatukumjulia hali mama.

Kinyume na matarajio tulipata sahani zilizofunikiwa kwa makawa. Ndani mlikuwa na mishumbi ya pilau na mchuzi rojorojo wa nyama. Tulifurikwa na kipeo cha furaha. "Wanangu, ndugu yenu sasa amepata kazi mjini. Mungu amemjalia kupewa mshahara mzuri. Kwa hivyo, hataki tena kuwaona, nyinyi wanuna wake, mkivalia masurupwete. Ameahidi kwamba hata karo yenu atawalipieni. Hamtataabika tena! Hatimaye, Mola ametushushia nyota ya jaha."

Maneno ya mama yalinishangaza sana. Kumbe kweli Lorenzo alikuwa kaka yangu? Kumbe imani yote aliyonionyesha muda wote nilipokuwa nikiuguza jeraha mkononi ilichochewa zaidi na udugu? Kwa nini muda wote huu haijanijia akilini kuwa Lorenzo ni kaka yangu? Ama ni kwa sababu ya tofauti ya kiumri kati yangu na yeye? Maswali haya na mengine mengi yalinigonga kichwani.

Lorenzo alikuwa ni kweli ndiye kifungua mimba katika aila yetu ya watoto tisa, ingawa mmoja alikuwa ashaaga dunia kutokana na ugonjwa wa kifua kikuu. Lorenzo alilelewa katika familia ya kina yakhe. Umaskini ulikuwa umetuvamia na kutuguguna kama vile mchwa wagugunavyo. Wanafunzi wenzake darasani waliotoka katika aila ya mabwanyenye hawakuchoka kumdhihaki na kumwuliza, "Kwani nyinyi na umaskini mlifunga pingu za maisha?" Lorenzo alikuwa hajitetei dhidi ya watesi wake. Aliuma meno na kujifariji kwa kusema kuwa, baada ya dhiki faraja hufuata.

Mungu hamnyimi mja vyote. Umaskini wa familia yetu haukumzuia Lorenzo kuwa na akili. Alikuwa fukara wa mali lakini tajiri wa akili. Shuleni alikuwa wembe; hakudiriki kuwa nambari nyingine ila moja na akitelcza nambari moja tu! Aliwashindia wenzake kwa mbali. Kutokana na kutolipiwa karo, mwalimu mkuu alimfukuza akachoka. Hapakuwa na haja yoyote ya kumtuma nyumbani, kisa na maana, si kuwa alisahau karo nyumbani, la hasha! Hatukuwa hata na rehe ya fulusi.

Lorenzo alijituma kufanya kazi za kijungujiko kama vile kupalilia mashamba ya wenye navyo, kuchuuza matunda, kubeba mizigo na kuwalishia watu mifugo. Kipato kidogo alichopata angekitumia kutufaa sisi aila yake. Alijitahidi kwa jino na ukucha. Matokeo ya mtihani wa kitaifa wa sekondari yalipotangazwa, Lorenzo alidhihirisha ujabali wake. Alifanikiwa kujiunga na chuo kikuu cha Inua.

Alipofuzu kutoka chuoni, milango ya heri ilifunguka. Alipata kazi ya uhasibu katika mojawapo ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali. Alianza kutufaa kwa chochote kile tulichotaka. Lorenzo aliwanunulia wazazi wangu kikataa cha shamba na akawajengea jumba la kifahari. Maisha katika familia yetu yalibadilika. Hadi sasa Lorenzo ni mtu mwadilifu na mcha Mungu. Sala za jioni aliziendesha yeye mwenyewe wakati wowote alipopata nafasi ya kujumuika nasi kijijini. Alitufunza thamani ya kuwa waadilifu na wakakamavu kazini.

Chambilecho wahenga, mcheza kwao hutuzwa. Kutokana na uadilifu na uaminifu wake, Lorenzo amepata kupanda daraja moja baada ya jingine katika uongozi. Amekuwa amirijeshi wa vita dhidi ya ufisadi. Yeye ni kielelezo cha maafisa wa umma na hata mashirika ya kibinafsi ambao hupenda kuvuna wasikopanda. Hivi sasa yeye ni afisa mkuu mtendaji katika tume ya kukabiliana na ufisadi.

**41.** Katika aya kwanza, msimulizi;
A. alikuwa hamjui Lorenzo kabla ya mwaka wa elfu mbili na moja.
B. japo alimfahamu Lorenzo hakuamini kuwa alikuwa ni ndugu yake hasa wa damu.
C. alikuwa hamjui Lorenzo kutokana na mwingiliano aliokuwa nao na mabinamu.
D. alikuwa hajui hasa ni nani aliyekuwa ndugu na yupi aliyekuwa mkoi.

**42.** Maana ya kuwa na mwao ni;
A. kuwa na shaka B. kuwa na hakika
C. kuwa na habari D. kuwa na hamu

**43.** Kifungu kimedhihirisha kwamba;
A. kufika kwa watoto hao nyumbani mapema kulisababishwa na uhaba wa mlo uliokuwapo.
B. yalikuwa mazoea ya msimulizi na wenzake kupata sahani zenye viporo zimefunikiwa kwa makawa.
C. msimulizi na wenzake walikuwa hawajaliani maslahi nyumbani hata kidogo.
D. tendo la kutomjulia hali mzazi walipofika nyumbani lilikuwa ishara ya kukosa malezi mema.

**44.** Chagua maana ya, masurupwete kwa mujibu wa kifungu.
A. mavazi ya thamani kuu
B. mavazi yavaliwayo juu ya nguo nyingine kuzuia zisichafuke.
C. nguo zilizochakaa na kuchanikachanika.
D. nguo zenye ukubwa usio wa kawaida.

**45.** "Kumbe kweli Lorenzo alikuwa kaka yangu" inaonyesha kuwa msimulizi;
A. amehuzunishwa na ukarimu ulioonyeshwa na ndugu yake.
B. anasikitika kwamba udugu kati yake na Lorenzo ulikuwa unaharibika.
C. amehakikisha kwenye fikra zake kuwa anashangaa kwa kutojua ukweli hapo awali.
D. anathibitisha mawazoni kuwa alikuwa hajakosea tangu zamani.

**46.** Chagua tabia zake Lorenzo kwa mujibu wa kifungu.
A. Mwenye stahamala, anayependa kujitegemea.
B. Mkarimu, asiyeaminika kwao.
C. Anayejua mustakabali wake, mnafiki.
D. Jasiri, mdanganyifu.

**47.** Ni jibu lipi sahihi kulingana na kifungu?
A. Lorenzo alikuwa mtu mwadilifu wakati huo tu.
B. Lorenzo alikuwa hakosi kuziendesha sala za jioni wakati wowote ule.
C. Kando na uaminifu wake,maadili ya Lorenzo yamemwezesha kupanda sana kitaaluma
D. Lorenzo aliwanunulia wazazi sehemu ya shamba na wao wakajijengea jumba la kifahari

**48.** Ni ipi hapa haijatajwa kama mojawapo ya kazi ambazo Lorenzo aliwahi kuzifanya?
A. Ukondakta
B. Uchuuzi
C. Umanamba
D. Uhamali

**49.** Kauli, "Shuleni alikuwa wembe' imetumia tamathali gani ya usemi?
A. Tashbihi
B. Istiara
C. Nahau
D. Kinaya

**50.** Kichwa mwafaka zaidi cha taarifa uliyoisoma ni;
A. Ufisadi unastahili kukomeshwa
B. Kazi za kijungujiko
C. Matatizo na ufanisi
D. Ndugu wa kweli

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**